PUBLIC PROCUREMENT APPEALS AUTHORITY
Efficient and Fair Appeals Dispensation
PPAA
MAMLAKA YA RUFANI YA ZABUNI ZA UMMA

PPAA
Toleo Na: 07 Oktoba - Desemba 2025

# BULLETIN

UTOAJI RUFAA KWA UFANISI NA HAKI



*Katibu Mtendaji - PPAA*
*Bw. James Sando*

## PPAA yahimiza matumizi ya Moduli kwa wadau wa ununuzi wa umma

**MPENDWA msomaji wa Jarida hili karibu tena ujisomee toleo la saba (07) la Jarida la Mtandaoni kutoka Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) *"PPAA Bulletin"*. Jarida hili ni moja kati ya njia inazozitumia PPAA katika Mawasiliano ya Kimkakati ya kuuhabarisha umma juu ya shughuli mbalimbali zilizotekelezwa kwa kipindi cha miezi mitatu.**

Ninayo furaha kukuletea Toleo la Saba la PPAA Bulletin kwa kipindi kingine tena cha miezi mitatu (Oktoba–Desemba, 2025), kwa lengo la kukuhabarisha juu ya shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi tajwa.

Mbali na kutekeleza jukumu lake la msingi la kushughulikia malalamiko na rufaa zilizowasilishwa mbele yake kwa kipindi tajwa, PPAA imefanikiwa kutoa elimu kwa wadau wa ununuzi wa umma na umma kwa ujumla katika Mkutano Mkuu wa 16 wa Mwaka wa Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) unaofanyika kwa siku mbili (tarehe 19 – 20 Desemba, 2025) jijini Arusha.

Aidha, katika toleo hili, tumekuandalia habari mbalimbali zinazohusu utekelezaji wa majukumu ya PPAA katika kufikia malengo iliyokusudia kwa kipindi tajwa.

Karibu usome jarida hili ili ufahamu kwa undani PPAA na shughuli ilizozitekeleza katika kipindi cha miezi mitatu (Oktoba–Desemba, 2025) na kuendeleza ushirikiano imara katika utoaji rufaa kwa ufanisi, wakati na kwa haki kwenye sekta ya ununuzi wa umma.

***#Kazi na Utu, Tunasonga Mbele.***

***Karibu Sana***

# Munde atoa kongole kwa PPAA kusimamia Matumizi ya Moduli

## ■ Aelekeza elimu zaidi itolewe kwa wadau wa ununuzi nchini




*Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Mhandisi Mshamu Ali Munde (Mb.) akimsikiliza Mkuu wa Sehemu ya Sheria wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bi. Agnes Sayi alipotembelea banda la PPAA pembezoni mwa Mkutano Mkuu wa 16 wa Mwaka wa Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) uliofanyika kwa siku mbili (tarehe 19–20 Desemba, 2025) jijini Arusha. Wengine pichani ni watumishi wa PPAA.*

**NAIBU Waziri wa Fedha, Mhe. Mhandisi Mshamu Ali Munde (Mb.) ameipongeza Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) kwa kuendelea kuisimamia vyema Moduli ya Kupokea na Kushughulikia Malalamiko na Rufaa Kieletroniki ambapo imekuwa nyenzo kwa wazabuni wenye malalamiko na rufaa.**

Waziri Munde ametoa pongezi hizo wakati alipotembelea banda la PPAA pembezoni mwa Mkutano Mkuu wa 16 wa Mwaka wa Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) uliofanyika kwa siku mbili (tarehe 19 – 20 Desemba, 2025) jijini Arusha.

Kadhalika, Mhe. Munde ameitaka PPAA kuendelea kutoa elimu kwa wadau wengi zaidi hususan wazabuni ili waweze kuitumia moduli hiyo kuwasilisha rufaa zao kwa wakati.

> *Inaendelea ukurasa wa 2*

# Munde atoa kongole kwa PPAA kusimamia Matumizi ya Moduli

< Inatoka ukurasa wa 1

Nawapongeza PPAA kwa kuendelea kuisimamia vyema moduli hii ya kuwasilisha malalamiko na rufaa...... endeleeni kufanya kazi kwa bidii na kuendana na kasi ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan," amesema Mhe. Munde.

Akiongea kwa niaba ya Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando, Mkuu wa Sehemu ya Sheria PPAA, Bi. Agnes Sayi amesema kwa kipindi cha mwaka mmoja PPAA imekuwa ikipokea rufaa kati ya 55-60 na zimekuwa zikishughulikiwa zote kwa wakati.

"Mhe. Naibu Waziri kupitia moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa ina faida kadhaa ikiwa ni pamoja kuokoa muda na gharama, imerahisisha upatikanaji wa nyaraka, kutunza kumbukumbu pamoja na kuongeza uwazi na uwajibikaji katika michakato ya ununuzi na ugavi," amesema Bi. Sayi.

Aidha, Mkutano Mkuu wa 16 wa Mwaka wa Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi umewakutanisha wadau wa sekta ya ununuzi takribani 2,500 kutoka taasisi za umma na binafsi nchini pamoja na za nje ya nchi.

Mkutano huo umeongozwa na Kaulimbiu "Kujenga Wataalamu wa Usimamizi wa Mnyororo wa Ugavi wa siku zijazo: "Uongozi na Ubunifu".




*Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Mhandisi Mshamu Ali Munde (Mb.) akiangalia jarida linalozalishwa na Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) "PPAA Bulletin" wakati alipotembelea banda la PPAA pembezoni mwa Mkutano Mkuu wa 16 wa Mwaka wa Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) uliofanyika kwa siku mbili (tarehe 19–20 Desemba, 2025) jijini Arusha. Wengine pichani ni watumishi wa PPAA.*




BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti
Florida Mapunda

Mhariri
Gloria Tesha
Mwandishi wa TSN

Wajumbe
Agnes Sayi
Mohamed Makame
Humphrey Kisanga

Katibu
Nelson Kessy

Mawasiliano:
Katibu Mtendaji
5 Mkandarasi Place,
Ghorofa ya nne, 58
Barabara ya Lusinde,
S.L.P. 1385, 41104 Dodoma
Simu: +255 (0) 743505505,
Baruapepe: barua@ppaa.go.tz
es@ppaa.go.tz
Tovuti: www.ppaa.go.tz



*Mwenyekiti wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Jaji mstaafu Awadh Bawazir, baadhi ya wajumbe wa mamlaka hiyo na watumishi wakisikiliza wasilisho la Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando juu ya matumizi ya Moduli ya kupokea na rufaa zilizowasilishwa zilikuwa 171, kusikiliza malalamiko na rufaa kieletroniki. Wasilisho hilo limefanyika mwezi Novemba katika Ofisi za PPAA jijini Dodoma.*

# Wajumbe wa Mamlaka ya Rufani wanolewa Matumizi ya Moduli

**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imefanya mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe wa mamlaka hiyo juu ya matumizi ya Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa kielektroniki katika mfumo NeST.**

Akifungua mafunzo ya siku moja ya tarehe 26 Novemba, 2025 kwa baadhi ya wajumbe wa PPAA, Katibu Mtendaji wa mamlaka, Bw. James Sando amesema kuanzishwa kwa moduli kumekuwa na faida kwa wazabuni, taasisi nunuzi na PPAA kwa kurahisisha uwasilishaji wa rufaa zinazotokana na michakato ya ununuzi wa umma.

"Moduli hii ina faida mbalimbali zikiwemo, kupunguza gharama na muda kwa wazabuni wakati wa kuwasilisha malalamiko au rufaa, kuongeza uwazi katika mchakato wa ushughulikiwaji wa malalamiko na rufaa," amesema Bw. Sando.

Pamoja na mambo mengine, Bw. Sando ameongeza kuwa hadi Oktoba, 2025 kupitia Moduli hiyo malalamiko/ rufaa zilizowasilishwa zilikuwa 171, ambazo zilitokana na michakato mbalimbali ya ununuzi wa umma.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa PPAA, Jaji mstaafu Mhe. Awadh Bawazir ameipongeza PPAA kwa kuendelea kutoa elimu ya Moduli kwa wadau wa ununuzi wa umma kwani kuendelea kufanya hivyo ni kuisaidia jamii kuielewa moduli hiyo na kuitumia kwa ufanisi na kuongeza tija katika ununuzi wa umma.



*Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando akitoa somo kwa baadhi ya wajumbe na watumishi wa mamlaka hiyo jinsi Moduli ya kupokea na kusikiliza malalamiko na rufaa kieletroniki inavyofanya kazi. Mafunzo hayo yamefanyika mwezi Novemba katika Ofisi za PPAA jijini Dodoma.*

# PPAA yasisitiza Matumizi ya Moduli kwa wadau



*Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando akiwaeleza waandishi wa habari juu ya faida za matumizi ya Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa kieletroniki pembezoni mwa Mkutano Mkuu wa 16 wa Mwaka wa Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) uliofanyika kwa siku mbili (tarehe 19–20 Desemba, 2025) jijini Arusha.*

**SERIKALI kupitia Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imewasisitiza wadau wa ununuzi wa umma husuan wazabuni na taasisi nunuzi kuzingatia matumizi ya Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa ili kuwasogezea wananchi huduma karibu pamoja na kuokoa muda na gharama zisizo na ulazima.**

Msisitizo huo umetolewa na Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando alipoongea na waandishi wa habari katika banda la mamlaka hiyo pembezoni mwa Mkutano Mkuu wa 16 wa Mwaka wa Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) uliofanyika kwa siku mbili (tarehe 19 – 20 Desemba, 2025) jijini Arusha.

Bw. Sando amewasisitiza wadau hao wa ununuzi wa umma kufuata maelekezo ya serikali ya kutumia mfumo wa NeST ambapo ndani yake kuna moduli ya kuwasilisha malalamiko na rufaa, hivyo watumie fursa hiyo kuwasilisha malalamiko na rufaa zao kwani moduli hiyo inaokoa muda na gharama pamoja na kuongeza uwazi na uwajibikaji.

"Moduli hii imekuja baada ya PPAA kutafakari kutokana na mapungufu mbalimbali yaliyokuwa yanajitokeza wakati wa kusikiliza rufaa zitokanazo na michakato ya ununuzi wa umma ambapo zimekuwa zikiwasilishwa nje ya mfumo ya kidijiti ikiwemo, utunzaji hafifu wa kumbukumbu, gharama, ukosefu wa nyaraka kwa wakati," amesema Bw. Sando.

Bw. Sando ameongeza kuwa manufaa ya kutumia moduli ni kwamba mzabuni anaweza kuwasilisha malalamiko/rufaa yake bila kufika ofisi za PPAA, inapunguza gharama na muda pamoja na uwazi, pia mzabuni anaweza kuona rufaa yake imefikia hatua gani na nyaraka zote zinapatikana katika mfumo wa NeST, jambo linalochangia uwazi zaidi.

PPAA imeunganisha taasisi nunuzi zote nchini kwenye mfumo ambapo mzabuni anaweza kuwasilisha rufaa yake katika taasisi nunuzi husika, baada ya kuwasilisha rufaa hiyo, PPAA ina uwezo wa kuona nyaraka zote zinazotumika katika mchakato mzima.

Hatua nyingine iliyobaki ni kuhakikisha moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa kuunganisha mfumo huo na mfumo wa mahakama ambapo zoezi hilo litafanyika katika mwaka wa fedha ujao.

Lengo la kuunganisha mifumo ni kuwasogezea huduma stahiki kwa wananchi kwa wakati kama ilivyosisitizwa katika dira ya 2050 ambapo inasisitiza kuwekeza katika matumizi ya Tehama ili kuwasaidia wananchi kupata huduma kwa uharaka na wepesi zaidi.

Bw. Sando amesisitiza taasisi za umma, wazabuni na wadau wa ununuzi wa umma kutumia moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa ili kuwasogezea wananchi huduma kwa wakati na kuisaidia serikali kupata thamani halisi ya fedha.

Pamoja na mambo mengine, Bw. Sando ametoa rai kwa wadau wa ununuzi kujitahidi kuhudhuria mafunzo ya matumizi ya moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa kieletroniki yanayoratibiwa na mamlaka hiyo kuanzia Januari 2026 katika mikoa mbalimbali nchini.

Awali akifungua Mkutano Mkuu wa 16 wa Mwaka wa Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) Naibu Waziri wa Fedha, Mhandisi Mshamu Ali Munde (Mb) kwa niaba ya Waziri wa Fedha, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb), amewataka wataalamu wa ununuzi na ugavi nchini kuongeza ubunifu, uongozi bora na matumizi ya teknolojia za kisasa ili kuongeza ufanisi, uwazi na tija katika matumizi ya fedha za umma.

Mhandisi Munde amesema hayo wakati akifungua Mkutano Mkuu wa Mwaka wa 16 wa Wataalam wa Ununuzi na Ugavi wenye kaulimbiu isemayo: "Kukuza Wataalam wa Usimamizi wa Mnyororo wa Ugavi watakaojiimarisha katika Ujuzi wa Uongozi na Ubunifu" ulioandaliwa na Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB), katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC), jijini Arusha.

Mhe. Mhandisi Munde, alisema serikali imejipanga kuimarisha usimamizi wa manunuzi kupitia Mfumo wa Kidijiti wa Ununuzi wa Umma, maarufu NeST, ili kupunguza gharama za ununuzi, kuongeza uwazi, kasi ya utekelezaji, kuzingatia bei ya soko, na kuleta tija kwa taifa.

"Serikali imeelekeza shughuli zote za ununuzi zifanyike kupitia mfumo wa NeST ili kuongeza uwazi, kupunguza gharama, na kuhakikisha thamani halisi ya fedha inapatikana katika miradi ya maendeleo," alisema Mhe. Mhandisi Munde.



# Wataalamu wa ununuzi na ugavi wapewa mbinu, faida kutumia NeST

**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imewanoa wataalamu wa ununuzi na ugavi nchini juu ya matumizi ya Moduli ya Kupokea na Kushughulikia Malalamiko na Rufaa katika mfumo wa NeST ili kuokoa muda na gharama zisizo na ulazima.**

Akitoa wasilisho katika Mkutano Mkuu wa 16 wa Mwaka uliofanyika jijini Arusha, Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando amesema serikali imetia msisitizo wa kuwasogezea wananchi huduma kwa karibu, hivyo kutumia moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa ni kuunga mkono jitihada za serikali.

Amewasihi wataalamu hao kutumia moduli hiyo pindi wanapopata changamoto au kutoridhika na michakato ya ununuzi wa umma.

Pamoja na mambo mengine, Bw. Sando pia aliwaeleza wataalamu hao faida zitokanazo na matumizi ya moduli hiyo kwamba inaokoa muda, gharama, kuongeza uwazi na uwajibikaji katika michakato ya ununuzi wa umma.

Bw. Sando amewasihi wazabuni kuitika wito wa serikali wa kutumia mfumo wa NeST ambapo ndani ya mfumo huo kuna moduli ya kuwasilisha malalamiko na rufaa, hivyo watumie fursa hiyo kuwasilisha malalamiko na rufaa zao.

“Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko katika mfumo wa NeST ni suluhisho kwa wazabuni katika kuwasilisha rufaa pindi wanapokuwa hawajaridhishwa na mchakato wa ununuzi wa umma katika zabuni walizoshiriki,” amesema Bw. Sando

Aidha, ameongeza kuwa manufaa ya kutumia moduli inamuwezesha mzabuni kuwasilisha malalamiko/rufaa yake bila kufika ofisi za PPAA, inapunguza gharama na muda pamoja na kuwa na uwazi, mzabuni anaweza kuona rufaa yake imefikia hatua gani na nyaraka zote zinapatikana katika mfumo wa NeST, jambo linalochangia uwazi zaidi.




*Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando akiwasilisha mada kuhusu matumizi ya Moduli ya Kuwasilisha na Kushughulikia Malalamiko na Rufaa kwa njia ya Kieletroniki kwa wataalamu wa ununuzi na ugavi katika Mkutano Mkuu wa 16 wa Mwaka wa Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi uliyofanyika jijini Arusha, tarehe 19 – 20 Desemba, 2025.*

# PPAA yamzawadia mhitimu bora somo la utafiti



*Aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Omolo akitoa hutuba kwa wahitimu wa ngazi mbalimbali za fani ya ununuzi na ugavi kwenye Mahafali ya 14 Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) yaliyofanyika Oktoba 25, 2025 jijini Dar es Salaam. Kwa sasa Bi Omolo ni Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Maendeleo ya Vijana.*

**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imemzawadia TZS. 1,000,000/- mhitimu bora wa somo la Utafiti kutoka Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB).**

Zawadi hiyo imekabidhiwa kwa Bw. John Mlyakado katika Mahafali ya 14 ya PSPTB yaliyofanyika Oktoba 25, 2025 jijini Dar es Salaam.

Akikabidhi zawadi hiyo kwa mwanafunzi huyo, aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Omolo amewapongeza wahitimu wote na kuwasisitiza kuwa zawadi walizozipata ni motisha kwa wanafunzi wote wa fani ya ununuzi na ugavi baada ya kufanya vizuri katika masomo yao.

"Napenda kutoa rai kwa wanafunzi wengine pamoja na waliofanya vizuri katika masomo yao kuhakikisha mnatumia taaluma yenu vizuri ili kuisaidia jamii na serikali hususan katika sekta ya ununuzi na ugavi," amesema Bi. Omolo.

Awali katika hotuba yake, Bi. Omolo amewataka wahitimu kufanya kazi kwa uadilifu na weledi, akibainisha kuwa kufanya kazi ya ununuzi na ugavi bila taaluma husika ni ukiukwaji wa Sheria ya PSPTB Namba 23 ya Mwaka 2007.

Bi. Omolo kupitia mahafali hayo, ameelekeza waajiri wote wa sekta ya umma na binafsi nchini kuzingatia matakwa ya kifungu cha 11 cha sheria hiyo, ambacho kimeweka adhabu kwa wote watakaobainika kukiuka masharti yake.

"Naiagiza bodi kuendelea kusimamia utekelezaji wa sheria hiyo kwa kufanya ukaguzi katika sekta za umma na binafsi, na kuwabaini wote wanaoendelea kufanya kazi za manunuzi na ugavi bila kuwa na sifa stahiki za kitaaluma," amesema Bi. Omolo.

Hata hivyo, amewahimiza wahitimu hao kuendelea kujifunza katika vyuo mbalimbali duniani ili kukuza taaluma zao na kujiandaa kwa ushindani wa soko la ajira la kimataifa.

Kwa upande wake, mwanafunzi aliyefanya vizuri na kupewa kiasi hicho cha fedha Bw. John Mlyakado ameipongeza Mamkala ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) kwa kumzawadia zawadi hiyo na kuongeza kuwa imemfanya kuwa na motisha wa kufanya vizuri zaidi katika masomo yake ya ngazi ya juu na kuahidi atakuwa balozi mwema wa PPAA kokote atakapokuwa.



*Aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Omolo akimkabidhi zawadi ya cheti Mhitimu bora wa Somo la Utafiti Bw. John Mlyakado wakati wa Mahafali ya 14 Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) yaliyofanyika Oktoba 25, 2025 jijini Dar es Salaam. Kwa sasa Bi Omolo ni Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Maendeleo ya Vijana.*

# UCSAF yaamuriwa kufanya upya tathmini ya zabuni na sheria

**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imeridhia rufaa iliyowasilishwa dhidi ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), ikabatilisha Notisi ya Nia ya kutoa zabuni na kuiagiza pia kumrudisha mlalamikaji katika mchakato wa zabuni pamoja na kufanya upya tathmini ya zabuni kwa kutumia timu mpya ya tathmini na kwa kuzingatia sheria.**

Rufaa hiyo iliwasilishwa na kampuni ya Decuple Services Ltd juu ya zabuni ya ufungaji wa mabango ya tovuti 694 za UCSAF, baada ya kutoridhishwa na sababu zilizotolewa za kuiondoa kwenye mchakato wa zabuni, zikieleza zabuni yake ilishindwa kuonesha uzoefu wa jumla na mahususi uliotakiwa kama ulivyoainishwa katika nyaraka za zabuni.



Mlalamikaji alieleza kuwa alishiriki katika zabuni hiyo akiwa na uhakika kwamba alikuwa ametimiza masharti yote na sifa zilizohitajika lakini baadae alipokea notisi ya nia ya kutoa zabuni, ambayo iliainisha kushindwa kwake kukidhi vigezo vya uzoefu wa jumla na mahususi kama sababu ya kuondolewa kwenye mchakato wa zabuni.

Mlalamikaji aliendelea kueleza kuwa alikuwa na uzoefu wa jumla na mahususi uliotakiwa, jambo lililothibitishwa na kukamilisha kazi ya utengenezaji na ufungaji wa mabango katika tovuti 500 mwaka 2024 wa thamani ya TZS 115,000,000.00.

Aidha, mkataba huo uliambatishwa katika zabuni yake iliyowasilishwa kupitia mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST). Hivyo, alikuwa na mtazamo kwamba alikidhi kikamilifu sharti la uzoefu mahususi lililohitaji wazabuni kuonesha uzoefu kupitia angalau mkataba mmoja wa aina inayofanana wa thamani isiyopungua TZS 25,000,000.00. Kwa msingi huo, alidai kuwa UCSAF ilikuwa na uelewa kamili wa uzoefu mahususi unaohusiana na zabuni hiyo.

Kuhusu kigezo cha uzoefu wa jumla wa mikataba, mlalamikaji aliwasilisha mikataba miwili kama uthibitisho: wa kwanza akiwa na UCSAF, na wa pili akiwa na kampuni ya Demeter Financial and Insurance Services Ltd, wenye thamani ya TZS 70,750,000.00. Alieleza kuwa mikataba yote miwili ilikuwa ndani ya muda uliobainishwa katika nyaraka za zabuni na ilizidi kiwango cha chini cha thamani ya TZS 25,000,000.00 kama ilivyoainishwa kwenye nyaraka ya zabuni.

Kutokana na hoja hizo, mlalamikaji alisisitiza kuwa alikuwa na vigezo vya uzoefu vilivyohitajika na hivyo hakupaswa kuondolewa kwenye mchakato wa zabuni. Aliiomba PPAA kuagiza mlalamikiwa kufanya upya tathmini ya zabuni na baada ya hapo kumpa mlalamikaji mkataba.

Kwa upande wake, UCSAF ilikiri kuwa mlalamikiwa aliiondoa zabuni ya mlalamikaji kutokana na kutokidhi matakwa ya uzoefu wa jumla na mahususi. Mlalamikiwa alikiri kupokea malalamiko kutoka kwa mlalamikaji kupitia mfumo wa NeST akipinga sababu za kuondolewa kwake; hata hivyo, UCSAF haikuweza kuyashughulikia malalamiko hayo kutokana na changamoto za kiufundi ndani ya NeST.

Baada ya kupokea rufaa hiyo, mlalamikiwa alipitia upya ripoti ya tathmini na nyaraka zilizowasilishwa pamoja na zabuni ya mlalamikaji, na ilibainika kuwa mlalamikaji aliwasilisha mikataba miwili iliyokuwa ndani ya kipindi kilichobainishwa na ilizidi thamani ya chini iliyotajwa katika nyaraka za zabuni.

Vilevile, baada ya kupitia nyaraka zilizowasilishwa kuthibitisha uzoefu mahususi wa mlalamikaji, ilionekana kuwa mkataba ulioambatishwa ulikuwa umetekelezwa kwa kiwango kikubwa, ukiwa umefikia zaidi ya asilimia 80 ya utekelezaji hadi tarehe 31 Desemba 2024.

Kwa kuzingatia matokeo hayo, UCSAF ilikubali rufaa hiyo na kuomba kufanyika upya kwa tathmini ya zabuni. Katika kuamua misingi ya rufaa hiyo, Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) ilibatilisha notisi ya nia ya kutoa zabuni na kuiagiza UCSAF kumrudisha mlalamikaji katika mchakato wa zabuni pamoja na kufanya upya tathmini ya zabuni kwa kutumia timu mpya ya tathmini, kwa kuzingatia kikamilifu sheria ya Ununuzi wa Umma.

# KIA yaamriwa kuanzisha upya zabuni kwa kuzingatia sheria

**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imekubali rufaa na kuiamuru Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kupitia Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA) kuanzisha upya mchakato wa zabuni kwa kuzingatia matakwa ya sheria.**

Rufaa hiyo iliwasilishwa na Kampuni ya Bisech Investments Ltd baada ya kutoridhishwa na sababu za kuondolewa kwenye mchakato wa zabuni, ambapo zabuni yake ilienguliwa kwa madai kuwa uwezo wake wa kifedha ulikuwa chini ya kiwango kilichoainishwa katika nyaraka ya zabuni.

Mkata rufaa alidai kuwa mzabuni aliyependekezwa hakupaswa kupewa zabuni hiyo kwa kuwa hakukidhi vigezo vya uzoefu maalum na uzoefu wa jumla kama vilivyoelekezwa katika nyaraka ya zabuni.

Alirejea Kipengele cha 2 cha Sehemu ya IV "Vigezo vya Sifa na Tathmini", ambacho kilihitaji wazabuni kuonesha uzoefu maalum kwa kuwasilisha ushahidi wa utekelezaji wa mikataba mitatu, na katika mikataba hiyo mitatu angalau mkataba mmoja uwe umetekelezwa katika kiwanja chochote cha ndege nchini Tanzania kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja. Alidai kuwa mzabuni aliyependekezwa hakukidhi kigezo hicho kwa kuwa hakuwa na mikataba halali katika sekta ya anga, na hivyo zabuni yake ilipaswa kuondolewa.

Aliendelea kuwasilisha kuwa iwapo KIA ingefanya uchunguzi wa kina wa nyaraka zilizowasilishwa na mzabuni aliyependekezwa pamoja na mlalamikaji, angebaini upungufu wa uzoefu unaohitajika kwa upande wa mzabuni aliyependekezwa. Vilevile, angebaini uzoefu wa mlalamikaji katika sekta ya anga, jambo ambalo lingemfanya kuwa mzabuni aliyekuwa na sifa stahiki zaidi kupewa zabuni hiyo.

Kadhalika, mlalamikaji alipinga sababu za kuondolewa kwake kwa madai ya kushindwa kukidhi matakwa ya uwezo wa kifedha, akisisitiza kuwa alionesha kuwa na uwezo wa kutosha wa kupata rasilimali za kifedha.

Aliongeza kuwa nyaraka ya zabuni iliwataka wazabuni kuthibitisha upatikanaji wa rasilimali za kifedha zenye thamani ya Shilingi za Tanzania (TZS) 2,500,000,000.00. Katika kuthibitisha uwezo wake wa kifedha, aliwasilisha taarifa mbili za benki zilizoonesha salio la TZS 500,000,000.00 na TZS 200,000,000.00 kwa pamoja.

Kampuni ya Bisech Investments Ltd ilisisitiza kuwa, ingawa jumla ya TZS 700,000,000.00 ilikuwa chini ya kiwango kilichohitajika cha TZS 2,500,000,000.00, kiasi hicho kilikuwa cha kutosha kwa utekelezaji wa zabuni yenye thamani ya TZS 800,000,000.00. Alidai kuwa sharti la uwezo wa kifedha halikuwa halisi wala halikuwa la msingi, kwa kuwa halikuwa na uhusiano wowote na thamani ya mkataba wa zabuni husika. Alieleza kuwa KIA alipaswa kuweka sharti la uwezo wa kifedha linaloendana na thamani ya mkataba, badala ya kuweka kiwango kikubwa zaidi ya thamani ya mkataba kama kilivyoainishwa katika nyaraka ya zabuni.

Aidha, mlalamikaji alibainisha kuwa, alikuwa na sifa za kupewa zabuni hiyo kwa kuwa alinukuu bei ya chini ikilinganishwa na mzabuni aliyependekezwa kupewa zabuni. Alidai kuwa angepewa zabuni kungesaidia kuokoa fedha nyingi, ambazo zingeweza kuelekezwa katika shughuli nyingine za utekelezaji wa majukumu ya KIA.

Kwa upande wa KIA alidai kuwa nyaraka ya zabuni iliwataka wazabuni kuonesha uzoefu maalum wa kutoa huduma za usafirishaji wa wafanyakazi katika kiwanja cha ndege kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja. Ili kukidhi kigezo hicho, mzabuni aliyependekezwa kupewa zabuni aliwasilisha mkataba wa Kiwanja cha Ndege cha Dodoma, uliothibitisha kuwa alikuwa na uzoefu katika sekta ya anga. Hivyo, mzabuni aliyependekezwa alikidhi sharti la uzoefu maalum na alikuwa na sifa za kupewa zabuni hiyo.



Aliendelea kuwasilisha kuwa kwa mujibu wa nyaraka ya zabuni, wazabuni walitakiwa kuwasilisha ushahidi wa utekelezaji wa mkataba mmoja katika kiwanja kimoja cha ndege ndani ya kipindi cha kuanzia tarehe 1 Januari 2020 hadi 31 Desemba 2024. Katika mchakato wa tathmini, ilibainika kuwa mkataba wa mzabuni aliyependekezwa wa Kiwanja cha Ndege cha Dodoma ulisainiwa tarehe 26 Mei 2025 na ulikuwa wa kipindi cha mwaka mmoja. Alieleza kuwa, kwa kuwa hakuna mzabuni mwingine aliyekidhi kigezo hicho, KIA alitoa zabuni kwa mzabuni aliyependekezwa licha ya mkataba huo kutekelezwa nje ya kipindi kilichobainishwa. Alisisitiza kuwa mzabuni aliyependekezwa alistahili kupewa zabuni hiyo kwa kuwa mchakato wa tathmini ulizingatia matakwa ya kisheria, na hivyo kufanya uamuzi wa utoaji wa zabuni kuwa wa haki na halali.

Akijibu kuhusu hoja ya pili ya rufaa, KIA ilisisitiza kuwa zabuni ya mlalamikaji ilishindwa kukidhi kigezo cha uwezo wa kifedha kilichotaka wazabuni kuonesha uwezo wa kupata rasilimali za kifedha za thamani ya TZS 2,500,000,000.00, kama ilivyoainishwa katika nyaraka ya zabuni. Alieleza kuwa katika tathmini, mambo yaliyozingatiwa ni pamoja na ukwasi wa kifedha, mauzo, upatikanaji wa mikopo na uwezo wa jumla wa kutekeleza mkataba. Hivyo, mlalamikaji aliondolewa baada ya kubainika kuwa hakukidhi kigezo hicho.

Kuhusu sharti la TZS 2,500,000,000.00, KIA alisema kuwa kiwango hicho kiliwekwa ili kuhakikisha kuwa

mtoa huduma anayepata zabuni anakuwa na magari ya kuaminika na anaweza kuhakikisha utoaji wa huduma kwa wakati na kwa mwendelezo.

Alieleza kuwa kigezo hicho kiliwekwa kutokana na uzoefu wa awali ambapo ubora wa huduma ulidorora kutokana na uwezo mdogo wa mtoa huduma katika kufanya matengenezo ya magari kwa wakati. Aliongeza kuwa, ingawa zabuni hiyo ilikuwa na thamani ya TZS 800,000,000.00, kama alivyodai mlalamikaji, sharti la juu la uwezo wa kifedha lililenga kumpa KIA uhakika wa nguvu ya kifedha ya mzabuni.

Alisisitiza kuwa sharti la TZS 2,500,000,000.00 lilikuwa halisi wala halikuwa la kupindukia, kwani wazabuni wengine waliweza kulikidhi. Aidha, iwapo mlalamikaji aliona kigezo hicho kuwa hakifai, alipaswa kuomba ufafanuzi kabla ya tarehe ya mwisho ya kuwasilisha zabuni. Kwa kushiriki kwenye zabuni bila kuibua hoja yoyote, mlalamikaji alikubali kimyakimya masharti na vigezo vya zabuni.

Kuhusu madai ya mlalamikaji kuwa aliwasilisha bei ya chini, KIA amefafanua kuwa kuwasilisha bei ya chini pekee hakumaanishi kuwa mzabuni atapatiwa zabuni. Sheria ya Ununuzi wa Umma inataka mkataba utolewe kwa mzabuni mwenye zabuni iliyotathminiwa kuwa ya chini zaidi (lowest evaluated tenderer), si kwa yule aliyewasilisha bei ya chini tu. Kwa kuwa mlalamikaji aliondolewa katika hatua ya tathmini ya kibiashara kwa kushindwa kukidhi kigezo cha uwezo wa kifedha, zabuni yake haikuendelea katika hatua nyingine za tathmini, ikiwemo ulinganisho wa bei. Hivyo basi, hoja ya mlalamikaji katika suala hili haina msingi wowote.



Baada ya kupitia nyaraka zote, PPAA ilibaini kuwa kwa mujibu wa kifungu husika kilichotajwa, wazabuni walitakiwa kuonesha uzoefu maalum kwa kuwasilisha mikataba mitatu ya aina inayofanana, ambapo angalau mkataba mmoja ulipaswa kuhusisha utoaji wa huduma za usafirishaji wa wafanyakazi katika kiwanja chochote cha ndege nchini Tanzania. Kila mkataba ulitakiwa kuwa umetekelezwa kati ya tarehe 1 Januari 2020 hadi 31 Desemba 2024, na kuwa na thamani isiyopungua TZS 500,000,000.00. Baada ya kupitia mikataba iliyowasilishwa na mzabuni aliyependekezwa kupewa zabuni, ilibainika kuwa mikataba yote isipokuwa mmoja haikuhusu utoaji wa huduma za usafirishaji wa wafanyakazi katika kiwanja cha ndege, badala yake, ilihusu huduma za kukodisha magari, ambazo ni tofauti na mahitaji ya zabuni husika. Aidha, mikataba hiyo haikufikia thamani ya TZS 500,000,000/- kama ilivyoainishwa katika nyaraka ya zabuni.

Pia, mkataba pekee uliokuwa wa aina inayofanana na zabuni husika ni ule wa Kiwanja cha Ndege cha Dodoma wa utoaji wa huduma za usafirishaji wa wafanyakazi, uliosainiwa tarehe 26 Mei 2025, wa thamani ya TZS (ikiwemo VAT). Hata hivyo, kwa mujibu wa nyaraka ya zabuni, mkataba husika ulitakiwa kuwa umetekelezwa kati ya tarehe 01 Januari 2020 hadi 31 Desemba 2024 na kuwa na thamani isiyopungua TZS 500,000,000.00. Mkataba wa Kiwanja cha Ndege cha Dodoma ulisainiwa nje ya kipindi kilichobainishwa na thamani yake ilikuwa chini ya kiwango cha chini kilichohitajika. Kwa kuzingatia maelezo hayo, PPAA ilihitimisha kuwa mzabuni aliyependekezwa alishindwa kuonesha na kuthibitisha kigezo cha uzoefu maalum kama kilivyoainishwa katika nyaraka ya zabuni.

Katika kubaini iwapo mkata rufaa alikidhi sharti hili, Mamlaka ilipitia zabuni yake iliyowasilishwa kupitia mfumo wa NeST. Katika sehemu inayohitaji uthibitisho wa upatikanaji wa rasilimali za kifedha, mkata rufaa alitangaza kuwa ana "fedha taslimu na benki TZS 500,000,000.00" na akaambatisha taarifa ya benki kutoka Equity Bank Tanzania Ltd ya tarehe 27 Juni 2024, iliyoonesha salio la TZS 430,343,215.98. Aidha, mkata rufaa alitangaza kuwa ana upatikanaji wa mikopo (lines of credit) yenye thamani ya TZS 200,000,000.00 na akaambatisha taarifa nyingine ya benki kutoka Equity Bank Tanzania Ltd iliyoonesha salio la TZS 69,456,921.23 kwa kipindi cha kuanzia tarehe 23 Mei 2023 hadi 13 Juni 2023.

Kwa kuzingatia hoja hizo, PPAA ilibaini kuwa taarifa za benki zilizowasilishwa na mkata rufaa hazikukidhi kigezo cha upatikanaji wa rasilimali fedha kama kilivyoainishwa katika nyaraka ya zabuni. Hivyo, PPAA ilihitimisha kuwa kuondolewa kwa zabuni ya mlalamikaji kwa msingi huo kulikuwa na sababu za msingi na ilikuwa halali.

Mkata rufaa aliendelea kudai kuwa sharti la kuonesha uwezo wa kifedha wa kiasi cha TZS 2,500,000,000/= halikuwa halisi na halina mantiki. Ilibainika kuwa ikiwa mkata rufaa aliamini kuwa sharti hilo lingeathiri ushindani wa haki, alipaswa kuomba ufafanuzi kutoka kwa mlalamikiwa kabla ya tarehe ya mwisho ya kuwasilisha zabuni. Endapo KIA angeendelea na msimamo wake, mlalamikaji alikuwa na wajibu wa kuwasilisha malalamiko ndani ya siku tano za kazi tangu alipofahamu msimamo huo, kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma inayomtaka mzabuni kuwasilisha malalamiko kwa taasisi nunuzi mara moja baada ya kufahamu mazingira yanayosababisha malalamiko hayo.

Aidha, kuhusiana na hoja ya mlalamikaji kuwa aliwasilisha bei ya chini lakini zabuni ilitolewa kwa mzabuni aliyewasilisha bei ya juu zaidi, PPAA ilibaini kuwa hoja hiyo pia haina mashiko. Kama ilivyoainishwa hapo juu, mlalamikaji na mzabuni aliyependekezwa kupewa zabuni wote walishindwa kutimiza masharti yaliyoainishwa katika nyaraka za zabuni na hivyo walipaswa kutenguliwa. Hakuna hata mmoja wao aliyefika katika hatua ya tathmini ya kifedha, kwa kuwa zabuni zao zilikuwa hazikidhi masharti (non-responsive). Kwa sababu hiyo, hoja ya mkata rufaa katika kipengele hiki pia imekataliwa.

Kutokana na sababu zilizotajwa hapo juu, PPAA inamuamuru KIA kuanzisha upya mchakato wa zabuni kwa kuzingatia matakwa ya sheria.

# HABARI PICHA




*Naibu Waziri wa Fedha, Mhandisi Mshamu Ali Munde (Mb) akiwasilisha hotuba yake ya ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa 16 wa Mwaka kwa Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi, (hawapo pichani). Mkutano huo umefanyika kwa siku mbili (tarehe19–20 Desemba, 2025) jijini Arusha.*




*Mkuu wa Sehemu ya Sheria wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bi. Agnes Sayi akimkabidhi zawadi ya cheti mhitimu bora wa somo la Utafiti katika mahafali ya 14 ya mitihani ya Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) yaliyofanyika Oktoba, 2025 jijini Dar es Salaam.*



*Watumishi wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bi. Agnes Sayi na Bi.Ingah Ngonyani wakitoa elimu ya ununuzi kwa mdau aliyetembelea banda la PPAA wakati wa Mkutano Mkuu wa 16 wa Mwaka wa Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) wa tarehe 19 – 20 Desemba, 2025 jijini Arusha. Wengine pichani ni watumishi wa PPAA.*

# HABARIPICHA



*Mwenyekiti wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Jaji mstaafu Mhe. Awadh Bawazir, baadhi ya wajumbe na watumishi wa mamlaka hiyo wakisikiliza wasilisho la Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando juu ya matumizi ya Moduli ya Kupokea na Kusikiliza Malalamiko na Rufaa Kieletroniki mwezi Novemba, 2025 katika Ofisi za PPAA jijini Dodoma.*



*Naibu Waziri wa Fedha, Mhandisi Mshamu Ali Munde (Mb.) akimkabidhi tuzo Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando katika Mkutano Mkuu wa 16 wa Mwaka wa Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) wa tarehe 19 – 20 Desemba, 2025 jijini Arusha. Tuzo hiyo imetolewa na PSPTB kwa kutambua mchango wa PPAA kwenye sekta ya ununuzi wa umma.*



*Wakuu na wawakilishi wa taasisi zinazosimamia sekta ya ununuzi wa umma katika picha na meza kuu katika Mkutano Mkuu wa 16 wa Mwaka wa Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) wa tarehe 19 – 20 Desemba, 2025 jijini Arusha. Waliosimama wa kwanza kushoto ni Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando, katikati ni Mkurugenzi Mkuu wa PPRA, Bw. Denis Simba na mwisho ni Mwakilishi wa Afisa Mtendaji Mkuu wa GPSA.*

# HABARIPICHA




*Naibu Waziri wa Fedha, Mhandisi Mshamu Ali Munde (Mb) akiwasilisha hotuba yake ya ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa 16 wa Mwaka wa Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) uliofanyika kwa siku mbili (tarehe 19–20 Desemba, 2025) jijini Arusha.*




*Sehemu ya wadhamini wa mahafali ya 14 ya mitihani ya Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) katika picha na meza kuu wakati wa mahafali hayo yaliofanyika Oktoba, 2025 jijini Dar es Salaam.*



*Wadau wa sekta ya ununuzi wa umma kutoka Ukanda wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kumaliza kikao cha siku mbili mwezi Oktoba, Lusaka, Zambia.*